MOI anaonekana akihutubia kikao cha Umoja wa Mataifa New York.
PICHA: KENYA NEWS AGENCY

MOI akihojiana na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, York.
PICHA: KENYA NEWS AGENCY

Tuwacheni tutumie pesa zetu

NINGEPENDA kuwajibu mabibi waliyosema hawajaona harusi za mishumaa, harusi zetu ambazo watu wasema tunaiga makristo kwa kuvaa veli, ningependa muislamu au makristo yoyote aniambie katika kifungu gani cha Biblia kuwa makristo akiolewa velii? Au mahali gani katika Qurani imesema kuwa veli ni mavazi ya ki kristo wakati wa harusi?

Ninegependeleya mtu aniulize makristo gani alimvesha veli matoto wake akampeleka Hall na kumueka juu ya stage mbele za wanawake tuu, ambao walokuja kusherehekea hiyo harusi. Watu wanasema kuwa wakristo huvaa veli kuwa itakuwa ni sanda, ningependa kujua wapi haya yameandikwa?

Huku nikupenda kwa mtu binafsi tuu. Basi jamani ikiwa twataka kusherehekea harusi naikiwa wako wanawake kwenye harusi, na wamevaa nguo za hishema sioni ubaya wowote ikiwa mume atakuja kuchukua mkee wake na watu wa kamjua kuwa ni mume wafulani.

Wanazuoni wetu wanasema kuwa haya mambo ni uzushi haki kweli haya ni uzushi jambo lolote duniani lililozushwa watu wanalikataa naona baada hata ya kupanda gari tungekuwa tukienda kwa miguu maana kila kipya ni uzushi? Jamani kama tunataka kufanya sherehe, na kama tunazopesa za kufanya hizo sherehe basi kwa kidini tunaruhusiwa tafadhalini musifanye wivu.

Kama sasa mundadhani kuwa watu mwisho watabeba misalaba mtachoka sana

> ## SAUTI ZA WASOMAJI
> **COASTWEEK** Sanduku La Posta 87270, Mombasa KENYA

kungoja maana hayo hayatakuwa kwa Muislamu yoyote, kama hatutangoja sana basi pengine Bibi Farida na Bibi Maimuna watakuwa wamwanzo na wamwisho, wavunje recordi.

Ikiwa tukisherehekea harusi na tunaambiwa tunawaiga wakristo basi jamaa tusifanyeni kazi maofisini na kuvaa kanzu au waume zetu wawache kuvaa surwali na shati wavae vikoi waende kazini na kila pahali, hivyo kweli itawezekana?

Basi natuache wivu mtifurahishe kama tunauweza.

Zaitun Said Mohammed,
MOMBASA.

Askari wamegeuka maadui

KUHUSU maonevu tuyapatayo kwa Ant-poaching sisi raia wa Kiunga Division Lamu District ninamasikitiko makubwa kuona askari wote kutoka eneo hili hutumia uwezo wao kwa kupiga watu bure bila ya sababu yoyote. Na ni makosa ajabu kuona askari wakiwapiga watu badala ya kuwalinda.

Sisi watu wa Kiunga tulifukuzwa na mashifta na kupata hakikisho kwa serikali yetu tukufu kuwa tutalindwa. Mbona loo askari wetu wa Kenya walioletwa kutilinda wamebadilika kuwa adui zetu?

Tunaiomba serikaali yetu tukufu ifanye uchunguzi juu ya jambo kama hili maana huenda wakahatarisha maisha ya raia wa Kenya katika Division hii ya Kiunga ama si hivyo kuenda tukahama tena Kiunga.

Tunaomba kwa serikali yetu tukufu itusaidie kwa haraka.

S. Shallo,
LAMU

RAIS REAGAN AMSIFU SANA RAIS MOI - KAMA KIONGOZI MUHIMU AFRIKA

MUHESHIMIWA RAIS Daniel Arap Moi, amekuwa na shughuli nyingi sana muhimu za kiserikali, akiwa kama Mwenyekiti wa Nchi Huru za Afrika na pia akiwa kama Rais wa Nchi hii ya Kenya. Baada ya kumaliza Mkutano wa Kimataifa wa Nishati hapa Mjini Nairobi, aliruka hadi Mombasa kufungua maonyesho ya Kilimo. Na baada ya hafla hiyo alirudi tena Nairobi kwa hafla nyingine kama vile kufungua rasmi Maonyesho ya Kimataifa ya mwaka huu. Siku hiyo aliruka kuelekea Marekani kuhutubia Mkutano wa Umoja wa Mataifa akiwa kama mwenyekiti wa Nchi Huru za Afrika.

Huko Amerika, Mtukufu Rais alikitana na Reagan na kuzungumza naye miswada mabali ya kuleta manufaa ya mataifa haya mawili. Bwana Reagan, katika hotuba yake ya kumkaribisha Rais Moi, aliwahi kutamka kwamba Rais Moi kwa wakati huu ni kiongozi muhimu sana, kwa vile yeye ni Kiongozi wa sasa wa nchi Huru za Afrika na pia ndiye Kiongozi wa Serikali yetu ya Kenya, nchi ambayo yasifikana ulimwenguni kote kwa amani yake na ufanisi wake katika uchumi na biashara.

Maneno ya Rais Reagan kwamba Rais Moi ni mtu muhimu sana, ni lazima yatiwe manani na yathaminiwe na wakenya wote kwamba ni sifa ambayo imetolewa na kiongozi wa Taifa kubwa na tajiri katika ulimwengu. Sifa hiyo inaturudia sote Wakenya. Sifa hii na sisi raia kwa vile kudumisha amani. Yaani wakati Rais akiitisha mwito wa amani mapenzi na umoja, huwa lwngo la kuiweka Kenya katika mstari wa mbele katika nyanja za usalama.

Kwa hivyo ni muhimu sana wakati tunapopawa amri ya kudumisha amani, basi mara moja tufanye hivyo. Tukipawa amri ya kuwafikiria wengine katika nchi yetu, pia tuifate amri hiyo. Maana iwapo nchi yote ya Kenya itadumisha amani na raia wote wawe wanapendana na kusaidiana kama watu wa kabila moja tu bila ya kujali huyu ni nani, basi tukifnaya hivyo huwa tunamsaidia shida za mataifa mengine ambayo bado yakandamizwa na wakoloni katika Bara hili la Afrika.

Muheshimiwa Moi, akiwa kama Mwenyekiti wa Nchi Huru za Afrika ana wajibu wa kuleta maelewano mema na jirani zetu ili sote wananchi wa nchi hizi tatu za Afrika Mashariki tuishi kama ndugu kama hapo zamani. Na kwa hivyo ni wajibu wa kila kiongozi, akiwa mbunge bara ama waziri amsaidie Rais katika kazi yake hii muhimu ya maelewano bara zima la Afrika. Uishi Umoja wa Nchi Huru za Afrika.

Mungu ilinde Bara La Afrika.

KISWAHILI TU NDIYO LUGHA IWEZAYO KUTATUA TATIZO LA MAWASILIANO AFRIKA MASHARIKI

...HILI kama lugha nyingi... zote ulimwenguni ni ... kilicho hai. Kukua kwa ... hai na kiwe na afya ... mambo kadha ili uhai ... we wa manufaa kwake ... wale walionaye. Hali ... lugha yetu tukufu ya ...hili. Lugha yetu ya Kiswa... hai. Jambo ambalo sasa ... tujiulize uhai wa ... hi ni wa afya, ugonjwa ... au ulegevyo.

... wataalamu wote wa ... wanakubaliana katika ... moja muhimu katika ... ya umma kuwa hai, iwe ... na ipate kustawi ni ... huo umma wenyewe uwe ... na afya iwe chonjo ma... Hivi ni kusema kwamba ... kwa lugha kudhoo... kuenea kwake au ... kunyanyasika kwake ...gemea wale watumizi wa ... hiyo.

...tumizi wa lugha ya umma ... hai katika mambo yao ... kiutumaduni kiu... kiroho na umma huo ... na ari ya kutumia lugha ... bila shaka hiyo itakua ... pasavyo.

...AFARANSA

... zile nchi zilizokuwa ...waliwa na ufransa katika ... ambazo zina wananchi ... asili ya Uarabuni wali... kuitumia lugha ya ... katika shughuli zao za ... na utamaduni. Waliny... kweli kweli kwani ni ... wa kifransa kuwafan... waliowatawala wachu... na nyendo za Kifransa ... mwongozo wao unaojuli... asili ya "Assililation" ... uliowafanya wafransa ... kwa kidiri wali... Kiarabu na kwa kiasi ... muda walioweza ... kukieneza Kiarabu ... nchi zenye asili ya ... katika kontinenti ya ... huko kaskazini.

... imetumia vitabu, ... senema ma Idhaa ... lugha ya Kiarabu hata ... wenyewe waarabu wa ... ndio ikaweza kuzita... nchi za kiarabu ... mrefu mpaka hivi ... walipoiasi misri lakini ... nchi nyingi mno za ... zinategemea ujuzi ... Misri. Msingi wao ... wa hilo ni kwamba ... waliendesha lugha Kiarabu ... kwa njia kubwa na ... msingi imara iliyo ... sehemu.

NA FARAJ DUMILA

Msione ajabu sisi wananchi wa Kenya kuitegemea Tanzania katika matumizi yetu ya Kiswahili kwani ndugu zetu wa Tanzania wametangulia katika kustawisha vyombo vya uenezeji wa lugha. Tungekuw tukisoma kwa wingi magazeti yao ya Uhuru. Mzalwndo na nchi yetu lau yangekuwa yakitufikia nchini Kenya kwani ni magazeti yenye lugha fasaha yakiambatana halisi na utamaduni mila fikira nyendo na miundo ya maisha ya mtumiaji halisi Kiswahili. Ni Mswahili gani halisi asiyevutiwa na nyimbo za Unguja Kina Bakari Abedi WAnajulikana na kupendwa kote Kiswahili.

Leo kwa bahati nzuri kuna Idhaa nyingi ulimwenguni zinazo tangaza kwa Kiswahili na kwa hivyo msikilizaji anaouchaguzi wa kutosha wa kusikiliza pale anapofikiria patampatia matakwa yake ya habari wa kusikiliza nyimbo, hadithi fupi na hata habari za siasa zinazoaminika. Lakini mtu akifanya upelelezi mfupi ataona kwamba msikilizaji ni mwerevu na kila mwerevu kumpata kumpa utakalo naye atahitaji apate alitakalo kwako. Basi zile idhaa zinazofua na kutumia ujuzi wao huu kwamba wakitaka kuwapata wasikilizaji wengi katika ulimwengu unaoongea kisahili hawana budi kwanza kuwapatia watu hao yale mambo wanayoyapenda.

LUGHA FASAHA

Waswahili halisi wanapenda kiswahili fasaha kilicho tangamanishwa na mambo yanayowa husu wenyewe nyumbani kama kizo nyimbo za Twarabu zenye asili ya kimapenzi kiungwana kiuwlezaji wa kudidimia hadithi fupi zenye kugusia mizingira ya kinyumbani, siasa zenye kugusia asili yao. Ukitangamanisha haha na yale Idhaa hizo zinazotaka kuwafikia hao kwa hizo wao wanazoitia "Propaganda" bazini upesi kwa Idhaa hizo kuwateka nyara fikira za wasikilizaji hao pasi wenyewe kujua.

Hivi sasa serikali yetu ya Kenya ikishirikiana n Shirika la Umajoa wa Mataifa yaani 'UNESCO' inaanzisha magazeti ya ilayani ambayo madhumuni yake makubwa ni kuwapatia wananchi wa wilaya hizo wajipatie habari elimu na mambo ya utamaduni yanayowahusu wenyewe na pia magazeti hayo yawe ni chombo imara ya kuondoshelea mbali yule adui mkuu wa kutojua kusoma na kunadika.

Hivi sasa kuna magazeti matatu ya aina hiyo. Moja liko Kericho na linajulikana kwa jina la "Sauti ya Kericho", jingine like Meru nalo laitwa "Sauti ya Meru" na hivi majuzi tu jingine limebuniwa huko Kwale nalo laitwa "Sauti ya Kwale".

JISHINDIE
Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza maneno

SWAHILI CROSSWORD NO. 127

KWENDA KULIA:
1. Gazeti mashuhuri Afrika Mashariki
4. Abembeleza
6. Jimbo
7. Hikima, busara, bongo
9. Kiungo cha maneno
11. Harufu ya bahari
13. La chai au la kuogea
14. Mnyama wa ufuoni
15. Ama
16. Kama, mfano.

KWENDA CHINI:
1. Mkate wa kusukuma
2. Rahisi, nyepesi
3. Kinyume cha ezua
5. Toa habari au ilani
8. Bara Hindi
10. Mnyama wa kufuga
11. Sinyaa, kupevuka kwa ugonjwa
12. Shahada ya elimu
13. Shahada ya elimu

JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 126

1] Mohamed D. Jillo Jarha, Sanduku la Posta 36, VOI

2] Zahra Qoyyan, Sanduku la Posta 97002, MOMBASA

3] Haji A. Barawa, Sanduku la Posta 54, MARIAKANI

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 126 —

KWENDA KULIA:

1. TANGAWIZI, 8. DOA, 9. BAO, 10. ODA, 11. IMO, 12. ANAO, 14. KABA, 15. RAJ, 16. KURO, 18. NJAA, 21. IMO, 22. UGO, 23. MBU, 24. TAA, 25. AUMBULIWA.

KWENDA CHINI:

1. TANA, 2. NDOA, 3. GODORO, 4. AAA, 5. IBIA, 6. ZAMBIA, 7. IOOA, 13. NYUMBU, 14. KINGAL, 16. KIMA, 17. ROUM, 19. JOAI, 20. AGUA, 22. UTU.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayo kubalIwa.

Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LIMITED*, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 7.10.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.